

### **Muhtasari kwa Lugha Nyepesi wa Sera la Msaada wa Kifedha**

Metro itatoa huduma za afya za dharura au muhimu ya bure au katika viwango vya punguzo kwa wagonjwa ambao hawana bima au wana uwezo mdogo wa bima zilizopo. Kwa ujumla, wagonjwa wanaotosheleza punguzo lazima wawe na mapato ya familia chini ya 250% ya Miongozo za Shirikisho Kuhusu Umaskini, wakati wagonjwa wenye haki za huduma za bure lazima wawe na mapato ya familia chini ya 175% ya Miongozo za Shirikisho Kuhusu Umaskini. Msaada wa Kifedha pia inaweza kupatikana katika hali nyingine mdogo, kulingana na ukubwa wa deni za matibabu ya mgonjwa na kama mgonjwa anatimiza baadhi ya vigezo vingine kwa uhakiki.

Wagonjwa wanaotafuta msaada wa kifedha wanaweza kuomba kwa kukamilisha Ombi la Msaada wa Kifedha. Nakala za Ombi la Msaada wa Kifedha pamoja na Sera la Msaada wa Kifedha na Sera ya Malipo na Ukusanyaji zinapatikana <https://metrohealth.net/about-metro-health/billing-payment-options/financial-assistance/>. Wagonjwa wanaweza pia kuomba nakala ya bure ya Ombi la Msaada wa Kifedha na sera zilizotangulia kwa barua, kwa kupiga simu 616-252-7110 au 1-800-968-0051, au wanaweza kupata nakala ya bure binafsi kutoka kwa Mshauri wa Kifedha au Keshia katika Mapokezi ya Hospitali ya Metro Health (karibu na Dawati ya Usajili ya mgonjwa) au kwa Dawati yoyote ya Usajili ya mgonjwa katika eneo lolote la Metro. Msaada wa Ombi la Kifedha na sera yaliyotangulia (pamoja na huu muhtasari kwa lugha nyepesi) inapatikana kwa Kiingereza, Kihispania, Kiarabu, Kibosnia, Kiburma, Kichina -Mandarini, Kinepali, Kinyarwanda, Kikorea, Kisomali, Kiswahili na Kivietinamu

Ombi la Msaada wa Kifedha yaliopakamilika lazima yawasilishwe kwa Hospitali ya Metro Health, Kwa: Customer Service Office, PO Box 913 Wyoming, MI 49509-0913. Ombi yanaweza kupelekwa binafsi kwa Mshauri wa Kifedha au Keshia katika Mapokezi ya Hospitali ya Metro Health (karibu na Dawati la Usajili ya mgonjwa) au kwa Dawati lolote la Usajili ya mgonjwa katika eneo lolote ya Metro. Ombi pia inaweza kutumwa kwa barua ya Posta ya America kwa anwani hapo juu, au barua pepe kwa [CustomerService@metrogr.org](mailto:CustomerService@metrogr.org).

Watu wanaotafuta habari zaidi au wanaohitaji msaada katika kujaza Ombi la Msaada wa Kifedha wanaweza kuwasiliana na moja wa Wakilishi wa Metro waliofunzwa katika Ofisi ya Huduma kwa Wateja katika (616) 252-7110 au 1-800-968-0051, Jumatatu - Ijumaa 7:30 am – 4:45 p.m.

Mgonjwa anayefuzu kwa msaada wa kifedha chini ya Sera la Msaada wa Kifedha ya Metro kwa heshima ya huduma za dharura au kiafya muhimu hatatozwa zaidi kuliko kiasi kwa ujumla kinachodaiwa na Metro kwa ajili ya huduma hiyo kwa watu binafsi ambao wana bima ya kulipia huduma hiyo.